# HOTUBA YA MHE. ANNA E. MGHWIRA, MKUU WA MKOA WA KILIMANJARO KATIKA SEMINA YA WASTAAFU WA PSPF YENYE KAULI MBIU KUWA MAFAO NI MTAJI KWA UWEKEZAJI SAHIHI ILIYOFANYIKA MKOANI KILIMANJARO - TAREHE 30/06/2O17

- **Ndugu Adam Mayingu, Mkurugenzi Mkuu wa PSPF;**
- **Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro;**
- **Wastaafu Watarajiwa wa PSPF;**
- **Watumishi wa PSPF;**
- **Waandishi wa Habari;**
- **Wageni waalikwa;**
- **Mabibi na Mabwana:**

Awali ya yote naomba niungane nanyi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha salama siku ya leo na kuweza kushuhudia tukio hili la kihistoria kwa Mfuko wa PSPF.

Natoa shukrani za dhati kwa Mfuko wa Pensheni wa PSPF kwa kuandaa programu hii ya mafunzo kwa ajili wanachama wake, na hasa kwa kuzingatia kuwa inalenga kuwajengea uwezo wanufaikaji wa mafao ya uzeeni kuwa na maisha bora baada ya kustaafu. Kwa upande mwingine nawapongeza Wastaafu Watarajiwa kwa kukubali kwenu kuhudhuria semina hii. Hongereni sana.

Napenda kuwashukuru viongozi wote na wageni waalikwa mliopo hapa kushuhudia tukio hili la ufunguzi wa mpango wa mafunzo na fursa mbalimbali za uwekezaji kwa wanachama wanaokaribia kustaafu kwa mkoa wa Kilimanjaro.

Natambua kuwa kulipwa mafao ya uzeeni ni jambo moja na namna ya kutumia mafao hayo ni jambo jingine. Lakini kwa upekee kabisa PSPF mmeona pamoja na kuwa mmetekeleza jukumu lenu la kulipa mafao, mna wajibu wa kuhakikisha kuwa Mwanachama wenu anapata mwanga utakaomuongoza kutumia kwa njia sahihi fedha za mafao baada ya kustaafu.

**Mkurugenzi Mkuu na wageni waalikwa;**

Kwa mara ya kwanza nilisikia mpango huu wakati ulipofunguliwa na Makamu wa Rais, Mhe. Samia Suluhu Hassa tarehe 3 Juni, 2017 katika ukumbi wa Chuo cha Benki Kuu Mwanza na nafarijika kuona mmetimiza yale mliyoyaahidi siku ya ufunguzi.

**Mkurugenzi Mkuu na wageni waalikwa;**

Nimefurahi pia kusikia kuwa PSPF mnaendelea kutimiza azma ya serikali ya kuhakikisha Watanzania wengi zaidi wanajiunga na hifadhi ya jamii. Pamoja na mpango wa lazima kwa waajiriwa walioko katika sekta rasmi, PSPF mna mpango wa Hiari ambao kwa kiasi kikubwa umekuwa kivutio kwa Watanzania walioko katika sekta isiyo rasmi. Mpango huu wa hiari unawezesha wanachama wanaojiunga kunufaika na mafao mbali mbali kama vile **fao la ujasiriamali, fao la elimu na hasa huduma za matibabu** ambayo ni ya muhimu **sana kwa wananchi.** Kwa hakika mafao haya yote yanajibu changamoto zinazoikabili sekta isiyo rasmi. Wito wangu kwenu ni kuendelea kuwa wabunifu ili muendelee kubuni mafao zaidi yanayolilenga kundi hili la Watanzania. Hakika kwa kufanya hivi mtaendelea kuwavutia hata wale ambao hawajajiunga ili waweze kunufaika na hifadhi ya jamii.

**Mkurugenzi Mkuu na wageni waalikwa;**

Mtakumbuka kwamba mwelekeo wa serikali ya Awamu ya Tano ni kuipeleka Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo 2025. Eneo mojawapo litakalofanikisha azma hii ni uwekezaji katika viwanda vidogo na vya kati. Naiona fursa hii katika mpango huu wa PSPF kwani mafunzo haya yanalenga maeneo ya uwekezaji katika viwanda vidogo vidogo na vya kati, kilimo, biashara na ufugaji, pamoja na soko la fedha. Ni wazi mpango huu ukifanikiwa utajenga msingi imara wa kutumia mafao yanayolipwa na Mifuko ya pensheni kama chanzo cha mitaji ya kutekeleza miradi mbalimbali midogo midogo na **mikubwa** hivyo kukuza **kipato** cha Watanzania na kuongeza fursa za ajira hasa kwa vijana wetu.

**Mkurugenzi Mkuu na wageni waalikwa;**

Ninauona mchango wa PSPF katika maendeleo ya sekta ya hifadhi ya jamii na ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Kama mlivyoeleza kwenye hotuba zenu, PSPF ni Mfuko wa Pensheni wenye wastaafu wengi kwa mwaka na pia idadi kubwa ya wanaopokea pensheni ya kila mwezi. Semina hii itawajengea uwezo wa namna bora ya kutumia mafao yao ili kuepuka matumizi yasiyo na tija ya mafao yanayopelekea mstaafu kuwa na maisha magumu muda mfupi baada ya kupata kiinua mgongo kutokana na kukosa weledi katika

uwekezaji au kuwa na uchaguzi mbaya wa miradi. Niwapongeze washirika wote wa PSPF mliokaa pamoja na kuja na programu hii. Kwa kuzingatia ukubwa wa PSPF hususani idadi ya wanachama na mafao wanayolipa kwa wanachama, ni dhahiri kwamba matokeo ya mpango huu yataanza kuonekana baada ya muda mfupi tu wa utekelezaji wake.

Kiasi cha mafao kinacholipwa ni kikubwa na iwapo wastaafu wa PSPF wataelimishwa, fedha hizi zinaweza kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya uchumi na kuongeza fursa za ajira.

**Mkurugenzi Mkuu na wageni waalikwa;**

Fursa zitakazoibuliwa na mpango huu, zitatoa mwanya mkubwa kwa Wastaafu wa PSPF kuwekeza katika maeneo mbali mbali hasa baada ya kupata elimu katika mafunzo haya.

Elimu kuhusu namna ya kuanzisha au kuendeleza viwanda vidogo vidogo na vya kati, ni muhimu kwani sekta ya Viwanda Vidogo ni chachu katika kuendeleza viwanda nchi nzima. Kwa kuwa viwanda hivyi vitaenea hadi vijijini, pamoja na faida nyingine, vitapunguza wimbi la wananchi kutoka vijijini kuhamia mijini na kuongeza soko la malighafi inayozalishwa huko vijijini.

Aidha, itakuwa jambo jema kama washiriki wataamua kuwa na vikundi vya pamoja vya uwekezaji, ili waweze kuunganisha mitaji yao na kumiliki viwanda vya kati na viwanda vikubwa.

**Mkurugenzi Mkuu na wageni waalikwa;**

Binafsi natambua pia PSPF ina mipango mingine ya mikopo kwa wastaafu kama vile mikopo ya pensheni (Pension Advance) ambapo mstaafu anaweza kukopa hadi kiasi kinacholingana na pensheni ya mwaka na mkopo wa muda mrefu kupitia mabenki. Hakika hili ni jambo jema sana na PSPF mnastahili pongezi nyingi. Hongereni sana na endeleeni kuchapa kazi.

Napenda kutoa wito kwa Mifuko mingine kufuata mfano huu mzuri wa PSPF wa kutoa elimu kwa wastaafu watarajiwa, hususan kwa kuwaunganisha na taasisi zitakazowapatia utaalamu ili wanapoingia katika shughuli za ujasiriamali na uwekezaji, waweze kuyafanya yote wakiwa na dira ya kuwaongoza.

**Mkurugenzi Mkuu na wageni waalikwa;**

Naamini Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa PSPF inatimiza majukumu yake vyema na itausimamia Mfuko huu na Mifuko mingine yote kwa karibu sana, kuhakikisha kuwa michango ya wanachama iko salama muda wote.

Nawaasa watendaji wote wa PSPF kufanya kazi kwa uadilifu ili kuhakikisha wanachama wenu, hususan wazee wetu waliotumikia Taifa hili kwa uadilifu wanapata haki zao kwa mujibu wa sheria. Aidha nawasihi muendelee kuwa wabunifu katika kutoa huduma zenu ili kujenga Imani kwa mnaowahudumia.

**Mkurugenzi Mkuu na wageni waalikwa;**

Kazi yangu hapa leo ni kufungua mafunzo haya muhimu kwa watumishi wetu ambao wanatarajia kustaafu, hivyo sasa ninatamka kwamba mafunzo haya nimeyafungua rasmi.

**Asanteni sana kwa kunisikiliza!**

**Mungu Ibaraiki Tanzania!**

**Mungu Ibariki PSPF!**

**Mungu wabariki wastaafu watarajiwa.**